# YAH: HOTUBA YA MGENI RASMI MH. MWL. KHADIJA NYEMBO, MKUU WA WILAYA YA MAGU KWENYE KILELE CHA MAADHIMISHO YA SHEREHE YA WIKI YA MAJI LEO TAREHE 22/03/2017 KATIKA KIJIJI CHA NG'HAYA

**Mhe.** Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya,
**Mhe.** Makamu M/kiti wa Halmashauri ya Wilaya,
**Mhe.** Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu, Afya na Maji,
**Mheshimiwa** Diwani Kata ya Ng'haya
**Ndugu** Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya
Wakuu wa Idara ya Serikali,
Viongozi mbalimbali
Watumishi na wataalam wa Halmashauri,
Wananchi na wadau wote wa maji
Mabibi na mabwana
**Asalaam alaikuum**
**Bwana asifiwe**

Awali ya yote napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru sana kwa kunipa fursa hii kuwa mgeni rasmi katika sherehe hii ya kuadhimisha kilele cha sherehe ya wiki ya maji mwaka huu yenye maudhui **''Maji safi Na maji taka – Punguza uchafuzi yatumike kwa ufanisi''**. Vilevile napenda kuwashukuru wadau wote (Wageni waalikwa wote) kwa kuhudhuria kwenu kwenye sherehe hii ya maadhimisho haya muhimu ya sherehe za kilele cha wiki ya maji leo hapa katika kijiji cha Ng'haya ambayo kimkoa mwaka huu inaadhimishwa **Wilaya ya Ukerewe**.

Kadharika napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa uongozi wa Halmashauri ya Wilaya kupitia Idara ya Maji kwa kushirikiana sana na uongozi wa kijiji cha Ng'haya na kamati ya mradi wa maji wa kisima kwa kunikaribisha mimi binafsi na wadau wengine wote ili kwa pamoja tusherekee na kuadhimisha sherehe hii pamoja. Kwa moyo wa dhati nawashukuru na kupongeza uongozi wa Kamati ya Maji ya kisima, Kijiji, Kata, na Halmashauri ya Wilaya kupitia Idara ya Maji kwa juhudi na maandalizi yenu mazuri.

**Mhe. Mwenyekiti,** Maadhimisho haya ni muhimu sana katika kujadili na kutathamini mafanikio na changamoto mbalimbali na ndio maana tunaona yameshirikisha wadau muhimu mbalimbali kwa maslahi ya wana Magu na taifa letu kwa ujumla. Aidha ni jukumu la wadau wote kutathmini, kujadili, na kuweka mipango na mikakati mbalimbali ya kushughulikia na kukabiliana na changamoto za upatikanaji wa maji kiwilaya.

**Mhe. Mwenyekiti,** Kiwilaya Halmashauri ya wilaya ya Magu imekuwa ikifanya jitihada ya kujenga miradi mbalimbali ya maji (kama vile miradi ya Majibomba, visima virefu, matanki ya kuvuna maji ya mvua na malambo) ili kukabiliana na changamoto ya uhaba na upatikanaji wa maji.

Aidha sambamba na hilo Halmashauri ya Wilaya kupitia Ofisi ya Mhandisi wa Maji (W) imekua ikitoa mafunzo ya mbalimbali ili kuzijengea uwezo kamati za maji kwa mujibu sera ya maji ya mwaka 2002 na Sheria ya huduma ya maji Na. 12 ya mwaka 2009 vifungu vidogo Na. 31-34 vyote vinasisitiza jamii/ watumiaji maji kumiliki miradi ya maji na kusimamia utunzaji, uendeshaji na matengenezo ili kuwa na huduma ya maji endelevu.

**Mhe. Mwenyekiti na Wadau wengine,** Yapo mafakio mengi yamepatikana. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na

i. Serikali kupata fedha kwa ajili wa Mradi mkubwa wa Maji bomba wa Magu mjini ambao tayari Mkandarasi yupo site tayari kwa kuanza kazi. Mradi huu utahudumia mji wa Magu mjini na maeneo mengine ya vijiji jirani.
ii. Kukamilika kwa mradi wa maji bomba Nyanguge- Muda ambao tayari hadi sasa unafanya kazi na unahudumia vijiji 3 vya Nyanguge, Muda na Bugumangala.
iii. Kujenga mradi wa maji bomba Lugeye – Kigangama. Tayari mradi huu upo kwenye hatua ya mwisho kukamilika ujenzi, Tayari mradi umeanza kufanyiwa majaribio ya kusukuma maji kwa wananchi na unahudumia vijiji 3 vya Lugeye, Kigangama na Kitongosima.
iv. Uchimbaji wa visima wa visima virefu 17 na mioundombinu ya maji Lubugu, Kisesa B, Misambo and Yichobela**,**

Hata hivo Serikali yetu itaendelea kutafuta fedha kupitia wahisani na vyanzo vyake mbalimbali kwa ajili ya miundombinu ya maji kama vile visima, majibomba, matanki ya kuvuna maji ya mvua na malambo/ mabwawa. Sote tumesikia kuwa kisima hiki ni miongoni mwa visima 8 vilivyochimbwa kupitia program ya Maji vijijini na usafi wa mazingira (RWSSP). Visima vingine vimechimbwa katika vijiji mbalimbali katika wilaya yetu. Jukumu la serikali ni kuhakikisha kuwa inatafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji ili kutoa huduma ya maji safi na salama katika maeneo mbalimbali.

**Mhe. Mwenyekiti,** Niendelee kuwasihi na kuwaomba wadau wote wautunze mradi huu, kadharika nawasihi mutunze na kuhifadhi vyanzo vya maji kwa kupanda miti, kuacha kuchoma moto ovyo na kuhifadhi mazingira ili kuwa na maji ya uhakika na nishati inayozalishwa kutokana na maji kwa huduma endelevu.

**Mhe. Mwenyekiti,** Athari za kuharibika kwa mazingira zinaonekana dhahiri na ndio zinachangia kwa kiasi kikubwa uhaba wa rasilimali maji. Hali ya ukame imezidi, jua kali, maeneo mengine kuanza kuonekana kama jangwa, mabadiliko ya tabia ya nchi na sasa tunashuudia ukame ambao unaashiria uhaba mkubwa wa upatikanaji maji sio hapa Magu tu, bali ata sehemu kubwa ya nchi yetu na hizo ni baadhi tu ya dalili za uharibifu wa mazingira. Hivyo wadau wote tunajukumu kubwa la kutunza na kuhifadhi mazingira yetu ili kunusuru rasilimali maji isipotee.

**Mhe. Mwenyekiti,** Naendelea kusisitiza jamii na wananchi wote wanaozunguka na kuguswa na mradi huu kuwa tumepata bahati kubwa ya kuchimbiwa kisima hiki hapa katika kijiji chetu ambacho kitasaidia kupunguza uhaba wa maji kwa kiasi kikubwa katika shughuli zetu za kila siku, ni wajibu wetu sasa kukilinda na kukitunza vizuri ili kiwe endelevu na tuweze kufaidika nacho kuanzia sasa na siku za mbeleni**.**

**Mhe. Mwenyekiti** Napenda kumalizia kwa kuwashukuru na kuwapongeza tena viongozi, wataalam, watendaji wote, Kamati ya maji na wananchi wote ambao kwa namna moja ama nyingine wamefanikisha maadhimisho

ya sherehe hii ya wiki ya maji, Kazi hii haikuwa rahisi lakini kwa umoja na ushirikiano wao wamefanikisha vizuri, Nasema ahsanteni sana.
Nawatakia maadhimisho memema. Kwa hayo machache natamka na kutangaza kuwa sherehe hii nahitimisha rasmi leo katika wilaya ya Magu.
Maudhui ya mwaka huu ni ''**Maji safi Na maji taka – Punguza uchafuzi yatumike kwa ufanisi''**

**WIKI YA MAJI OYEEE!!!**

**NGHAYA OYEEE!!!**

**MAJI OYEEE!!!**

**Ahsanteni kwa kunisikilizi**